OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
MANISPAA YA UBUNGO
SHULE YA SEKONDARI MANZESE
Usajili No. S. 3250 ya Machi 15, 2007 : Motto: EDUCATION IS LIBERTY
Email:manzesesecumc@gmail.com
S.L.P 34602, DSM Mob: 0784-714822/0715-714822

TAREHE……..

Kumb na.UMC/MSS/S.3250/NO……..

Jina la Mwanafunzi (Majina matatu aliyefaulia)……..

FOMU YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Manzese mwaka 2021 kama mwanafunzi wa kutwa. **Hongera sana**.

MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya sekondari Manzese ipo mkoa wa Dar es salaam manispaa ya Ubungo,kata ya Manzese mtaa wa chakula bora .umbali kutoka barabara kuu ni kilometa moja na nusu(km 1.5)kutoka manzese darajani, barabara ya morogoro road.

MUDA WA KUFUNGUA SHULE

Shule itafunguliwa jumatatu tarehe **11/01/2021** saa 1:00 kamili asubuhi. fika na vitu vyote vinavyohitajika ili uweze kusajiliwa. Mwanafunzi ambaye hataripoti kwa muda uliopangwa nafasi yake itajazwa na mwanafunzi mwingine.

MAHITAJI MUHIMU YA MWANAFUNZI

- Begi jeusi la kubebea daftari.
- Mathematical set na kijitabu cha grafu
- Dictionary ya Oxford (English to English)
- Madaftari kumi na moja (Counter Book Q4 au Q3)
- Madaftari madogo ya msomo 11 yakufanyia mazoezi na majaribio.
- Faili la kutunzia mitihani yake
- Sare ya shule jozi mbili
- Saa ya mkononi ya kawaida(isiwe smart)
- Picha mbili na picha moja ya mzazi au mlezi(Njoo na picha na sio vinginevyo)
- Mkebe wa vifaa vya hisabati
- Kalamu ya wino na risasi pamoja na rula
- T-shirt rangi ya kijivu yenye kola(Form six) , bukta, truck suit rangi ya blue bahari na raba za kawaida nyeupe za kamba kwa ajili ya michezo(itavaliwa muda wa michezo siku ya jumatano tu na si vinginevyo) .

MAELEZO YA SALE YA SHULE

- Suruali /sketi mbili rangi ya blue bahari(Yenye rinda mbili) ,pindo la juu lenye upana wa Inch 18 chini.
- Soksi za rangi nyeupe jozi mbili
- Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na kisigino kirefu vya kufunga na kamba

- Nywele fupi sio kipara
- Shati jeupe mbili mikono mifupi isiyo bana na ndefu na ziwekewe alama ya I bega la kushoto(Tumia kitambaa cha sketi au suruali)
- Tai mbili rangi ya suruali/sketi
- Sweta la rangi ya blue bahari
- Mkanda mweuzi wa ngozi (usiwe na bakoli kubwa)
- Kitambaa cha mkononi cheupe(Pair mbili)
- Sweta rangi ya blue bahari
- Half kanzu kwa mwanafunzi anayo vaa hijabu,vanzi liwe refu na pana
- Shungi mbili za pamba nyeupe zisizokuwa na *mapambo na sketi ndefu na nusu kanzu mbili ndefu(* waislamu tu au wanao vaa hijjabu tu)
- Nywele fupi sio kipara

Mwanafunzi anatakiwa kuvaa nguo isiyobana, kwa wasichana nguo iwe ndefu

Ivuke magoti kwa cm 30

ANGALIZO

. sare ya shule ni alama ya shule, mwanafunzi ashone suruali yenye urefu stahili na upana usiopungua inch 16 na iwe nap indo la kuelejea juu. Shati iwe inayomtosha na ambayo atachomekea muda wote kwa wasichana na wavulana

. avae mkanda mweusi wa ngozi au usiwe na buckle kubwa, urembo au picha ya aina yoyote.

. mzazi /mlezi hakikisha mwanao habani shati, hijabu au suruali na kuifanya modal. Sare ya namna hii tutaiharibu kwa kuikata na kuichana.

Mwanafunzi akivaa vaa viatu, sweta, jaketi, au soksi tofauti kwa sababu maalum afike mapema asubuhi atoe taarifa na apewe ruhusa na mwalimu wa zamu , vinginevyo atanyang'an'wa bila maelezo yoyote bila maelezo ya aina yoyote viatu/soksi hizo na havitarudishwa.

.wasichana wanaovaa hijabu hawaruhusiwi kuvaa shati au T-shirt.

.wanafunzi wote wanatakiwa kunyoa nywele fupi na sio kipara au kiduku (ukibainika unafukuzwa shule)

. mwanafunzi akichelewa/kuruka uzio/akitoroka/utoro wa rejareja/kutokuchomekea shati la shule/kutokuvaa soksi/kutokuvaa mkanda/kuaa chooni/ kutokuwa na nukuu za somo/kucheza kamali/kubeti/kucheza vijumbe/kuwa na nywele ndefu na kusuka au kuharibu mali ya umma kwa makusudi atarudishwa nyumbanui na kumleta mzazi /mlezi wake na arudipo shuleni atalazimika kutekeleza maamuzi ya kikao cha wazazi cha tarehe 11/09/2020 na tarehe 29/09/2020.

. serikali inatoa elimu bure, haturuhusu michango ya aina yoyote(kila kitu nunua mwenyewe).

Wanafunzi wote wa kike wanatakiwa kupima afya zao mara kwa mara na kuwasilisha fomu inapofunguliwa shule baada ya kila likizo.

. mwanafunzi awe na chombo chake binafsi kwa ajili ya chakula /maji/chai ili kutunza afya yake.

. muda wa kuingia shuleni ni kuanzia saa 12.00 – 1.00 asubuhi, saa moja na nusu asubuhi masomo yanaanza rasmi hadi saa 11.00 jioni

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa walimu, viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b. Kila mwanafunzi lazima afanye bidii katika kila somo. Mwanafunzi ambaye atapata chini ya 50% atapata adhabu
c. Mahudhurio mazuri katika shughuli za ndani na nje ya shule ni muhimu
d. **Kutimiza** kwa makini kazi za shule na kufanyia nyumbani.
e. Mwanafunzi anatakiwa kusimama, kusalimia,na kuwapokea mizigo walimu au mtu yeyote mwenye umri mkubwa zaidi yake popote pale akutanapo na watu wa aina hiyo.
f. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopangiwa**.**
g. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo muda wote ukiwa shuleni.
h. Hairuhusiwi kutumia **LUGHA CHAFU** miongoni mwa wanafunzi wenzake, viranja na wafanyakazi wote wa shule.
i. Mwanafunzi lazima afanye mitihani ya masomo yote anayo soma shuleni hapo.
j. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule, mali zao binafsi na mali za shule. Pia wanatakiwa kutoa taarifa kwenye utawala juu ya uharibifu wa mali ya shule.
k. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
l. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
m. Adhabu ya viboko itaruhusiwa kwa kosa linalostahili na kuwa na taarifa/ kibali cha mkuu wa shule.
n. Hakikisha muda wote unapokuwa shuleni unaongea lugha ya **KINGEREZA** nje na ndani ya darasa.
o. Mwanafunzi yeyote atakae kamatwa na kitu chochote kisichotakiwa shuleni kitaharibiwa mbele yake.
p. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kwenda kwenye maeneo yafuatayo bila sababu maalumu au bila kupewa ruhusa.
    i. Shule za jirani na madukani
    ii. Nyumba zinazo zunguka shule
    iii. Vibanda vya biashara nje ya shule
    iv. Kukutwa nje ya eneo la shule kwa ujumla
q. Ni marufuku kwa mwanafunzi kukutwa sehemu zifuatazo:-
    i. Baa na klabu za usiku
    ii. Nyumba za kulala wageni isipokuwa wanapokuwa na wazazi au walezi wao

VITU VISIVYORUHUSIWA.

1. Pete, kunyoa nyusi, kuvaa hereni, kupaka hina,kupaka rangi kucha, kucha chafu, kutengeneza nywele kwa dawa, kunyoa mitindo, kuvaa viatu vinavyofanana na vya jeshi, kuvaa sendozi,kuvaa viatu vya mgogo(kanda mbili za tairi) na mikanda isiyofaa kuvaa nguo za kubana na kata' k',kuvaa nguo fupi, kuwa na simu, kamera, ipad, albam za picha na CD, matusi,kuwa na redio na kusuka nywele na kufuga ndevu,kuvaa kofia, kuvaa rozari, na kuvaa rubber/shanga(culture) mikononi.
2. Kuruka ukuta/uzio,ukibainika umetenda kosa hili utaadhibiwa kutokana na sharia zilizopo ikiwa kusimamishwa masomo.

B. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.

1. Wizi na unyang'anyi
2. Uasherati, ubakaji na ushoga
3. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya
4. Uvutaji bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana na kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kuoana au kuolewa
9. Kudharau bendera ya Taifa

10. Kutohudhuria shuleni kwa muda wa siku 30/90 mfululizo bila taarifa.
11. Kupata au kusababisha ujauzito
12. Kutoa mimba
13. Kugoma, kuchochea vurugu na kusababisha uvunjifu wa amani
14. Kukataa adhabu kwa makusudi.
15. Kukuwadia mwanafunzi mwenzie na mtumishi yeyote katka mambo ya mapenzi ndani na nje ya shule.
16. Kunyanyasa mwanafunzi mwenzie kutokana na jinsia yake, udini, ulemavu, ugeni wake au hali yake.
17. Kughushi mitihani au wizi wa mitihani, kukataa au kutofanya mitihani na mazoezi ya masomo bila sababu za msingi.
18. Kutokuwa na ripoti ya maendeleo yake ya nusu Mwaka au Mwaka n.k
19. Kuzomea watumishi au kuchokoza wanafunzi wengine na matumizi ya lugha chafu za matusi

C. WAJIBU WA MZAZI

1. Mzazi /mlezi anatakiwa kumleta mwanae kumwandikisha shuleni anapoanza masomo.
2. Mzazi/ mlezi anatakiwa kuandikisha majina ya watu wanne na namba zao za simu watakao ruhusiwa kupata ripoti za mtoto akiwa shuleni na mawasiliano ya vikao, wito, n.k
3. Mzazi/mlezi anatakiwa kuja kuchukuwa ripoti ya mtoto wake kwa muhula husika vinginevyo hatopokelewa kwa muhula unao fuata
4. Mzazi/ mlezi anatakiwa afike shuleni kwa muda muafaka pindi anapohitajika na uongozi wa shule
5. Mzazi/ mlezi ajenge tabia ya kutembelea shule mara kwa mara ili kujua maendeleo ya mtoto wake baadala ya kusubiri kuitwa ili kujenga mshikamano wa malezi.
6. Mzazi/ mlezi amfahamu kwa jina na namba ya simu mwalimu wa darasa la mtoto wake ili kujenga mahusiano ya malezi ya mtoto.
   Matumizi na mahitaji ya mwanafunzi inategemea zaidi wewe/ mzazi/ mlezi.

Ni imani yangu kuwa utampatia mwanao kila aina ya msaada ili aweze kusoma kwa makini.
Nijukumu la Mzazi/ Mlezi kumpatia mwanao matibabu pindi atakapo ugua siyo jukumu la shule.
Tafadhali soma kwa makini sana maelekezo hayo, shule haipo tayari kwa usumbufu.

MWISHO

Uongozi wa shule unakutakia maadalizi mema, ni matumaini yetu kuwa utazingatia kanuni, taratibu na sheria zote za shule.

……..
MWL.OMARI S. MWANGI
MKUU WA SHULE

MUHIMU:
Fomu zilizoambatanishwa zinatakiwa zijazwe kikamilifu na zirudishwe shuleni.

1. ***Fomu rasmi ya kuandikishwa***
2. ***Ahadi ya mwanafunzi na Mzazi/Mlezi***
3. ***Fomu ya uchunguzi wa Daktari***

FOMU RASMI YA KUANDIKISHWA

TAARIFA BINAFSI

Jina la mwanafunzi.....Tarehe kuzaliwa.....mwezi.....mwaka .....

SHULE YA MSINGI ALIYOSOMA.....KATA.....MWAKA.....

USAFIRI: MIGUU.....GARI MOJA.....GARI MBILI.....GARI TATU.....GARI NNE.....

UMBALI KUTOKA UNAPAISHI HADI SHULENI: KM 0-KM 3.....ZAIDI YA KM 3.....WEKA ALAMA YA'V' KWA USAFIRI ANAYO TUMIA KUFIKA SHULENI.

JINA LA MZAZI/MLEZI.....

Namba ya simu.....Mahali anapoishi.....

Mtaa/Kitongoji.....Kata.....Tarafa.....

Wilaya.....Mkoa.....

Anuani ya kudumu ya mzazi/mlezi.....

Uhusiano wako na mwanafunzi.....

Weka alama ya vema (V) panapohusika

Anaishi na wazazi wote wawili ( )

Anaishi na mzazi mmoja mataje ……

Yatima ( ) unaishi na nani …….. uhusiano …….

Majina mengine ya watu watatu(4) wenye uhusiano wa karibu na mwanafunzi ambao wataweza kutoa/kupewa taarifa ya maendeleo ya mwanafunzi au kuwasiliana nao wakati wa dharura.

S/NO	JINA LA NDUGU	ANAPOISHI	MAHUSIANO	ANUANI	NAMBA YA SIMU
1.					
2.					
3.					
4.					

KIAMBATANISHO "B"

AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi.....

1. Nimeyasoma na kuyaelewa maelezo yote na nimekubali kujiunga na shule hii ya sekondari manzese kuanzia tarehe 11/01/2018
2. Naahidi kwamba :-
   a. Nitazingatia sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyo tajwa.
   b. Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania
   c. Nitatunza mali ya Umma ambayo ni pamoja na Majengo, Samani, Sitaruka uzio au ukuta wa Shule, vitabu na vifaa vya maabara.
   d. Nipo tayari kuchukuliwa hatua yoyote stahiki endapo nitakiuka maelekezo yaliyotolewa kwenye fomu hii.

   Saini ya Mwanafunzi.....tarehe: .....

.....

AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mzazi/ mlezi wa .....kidato cha.....

Na ahidi kwamba:-

a. Nitashirikiana kikamilifu na uongozi wa shule na walimu wote kwa ujumla katika kumuelimisha na kumlea mtoto wangu. Hii ni kuhakikisha kuwa atatii kanuni, taratibu na sheria zote za shule na kuyazingatia mambo yote muhimu yaliyotajwa.
b. Nitafanya kila niwezalo kumwezesha mwanangu kufika shuleni kila siku kabla ya saa 1:00 asubuhi .
c. Na kwamba mwanafunzi atahitimu na kufuzu kidato cha kwanza hadi cha nne.
d. Ninaruhusu mwanangu achukuliwe hatua yoyote stahiki endapo atavunja mojawapo ya sharia, taratibu na kanuni zilizoorodheshwa.

   Saini ya Mzazi/mlezi.....tarehe: .....

KIAMBATANISHO A.

Unatakiwa ufanyiwe uchunguzi na daktari, uje na fomu iliyoambatanishwa ikiwa imejazwa kikamilifu na daktari wa Hospitali ya Serikali. Tafadhali usifiche tatizo lolote ili uweze kupata msaada.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION
AND LOCAL GOVERNMENT

MANZESE SECONDARY SCHOOL

Request for Medical Examination

To be filled by Government Medical Officer and return to the Head of School Manzese Secondary School,

To the Medical Officer,

……..

……

A. Re…….
Please examine the above mentioned student comment on his/her fitness by responding to the problems below say YES or NO to each problems and if YES then state.

Signature ……
HEAD MISTRESS/MASTER
Date ……

Insert (V) in the boxes provided

i.	**Hearing**	**YES ( )**	**NO ( )**
ii.	**Speech**	**YES ( )**	**NO ( )**
iii.	**Sight**	**YES ( )**	**NO ( )**
iv.	**T.B**	**YES ( )**	**NO ( )**
v.	**B.T**	**YES ( )**	**NO ( )**
vi.	**Diabetes**	**YES ( )**	**NO ( )**
vii.	**Mental case**	**YES ( )**	**NO ( )**
viii.	**Physical disability**	**YES ( )**	**NO ( )**
ix.	**Pregnancy**	**YES ( )**	**NO ( )**
x.	**Any**	**YES ( )**	**NO ( )**

Designation…….Signature……..Date……